# Mwanasheria Mkuu anavyosimamia upatikanaji haki, utekelezaji Dira 2050

Na Mwandishi Wetu

MOJA ya nafasi ya juu ya uongozi na nyeti nchini ni ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Hii ni kutokana na ukweli kuwa, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu imetajwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 Ibara ya 59 (1).

Jukumu kubwa la ofisi hii ni kuishauri serikali katika masuala yote ya kisheria ndani na nje ya nchi katika maeneo ya

uandishi wa sheria, urekebu wa sheria, ufasiri sheria, upekuzi na uchambuzi wa mikataba mbalimbali ya kiuwekezaji.

Aidha, ofisi hii inaiwakilisha serikali kitaifa, kikanda na kimataifa katika masuala yenye maslahi kwa taifa kama yalivyooneshwa katika Ibara ya 59 (3) ya katiba hiyo na yanaainishwa katika Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Sura ya 268.

Miongoni mwa majukumu hayo ni kuishauri serikali kuhusu masuala yote ya kisheria ikiwamo mikataba ya kimataifa ambayo

Tanzania ni sehemu ya mkataba ama ina maslahi katika mkataba hiyo.
Aidha, kutoa ushauri kwa wizara, idara zinazojitegemea na taasisi za serikali kuhusu mchakato wa utungwaji wa sheria na masuala mengine yahusuyo sheria, na kutoa ushauri stahiki wa sheria zilizotungwa na Bunge, sheria ndogo na maazimio mbalimbali na kuandaa miswada ya sheria kwa ajili ya kuwasilishwa bungeni.
Majukumu mengine ni kuandaa hati zote za kisheria na maazimio kwa ajili ya kuidhinishwa na Bunge, kushauri na

kudumisha uhusiano kati ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Taifa ya Mashitaka ili kuleta ufanisi kuhusu suala lolote lililopo mahakamani na katika mabaraza.

Lingine ni kupokea taarifa kutoka kwa Wakili Mkuu wa Serikali na Mkurugenzi wa Mashitaka ili kushauri Serikali, Bunge na Mahakama.

Aidha, kuwasimamia maofisa sheria na mawakili wa serikali wote walioko katika wizara, idara na taasisi za serikali katika kutekeleza majukumu yao ya kisheria, na

kushiriki katika kudhibiti nidhamu ya mawakili wa kujitegemea kupitia Kamati ya Maadili ya Mawakili.

Katika kutekeleza haya, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imefanya mambo mengi kuhakikisha majukumu yake yanaisaidia serikali katika eneo hili la kisheria.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Hamza Johari anazungumzia namna ofisi hiyo ilivyojipanga kwa miaka minne sasa ya Uongozi wa Awamu ya Sita chini ya Rais

Samia Suluhu Hassan kutekeleza majukumu hayo kikamilifu.

Katika mahojiano na vyombo vya habari ofisini kwake Mtumba mkoani Dodoma, anabainisha ushiriki wa ofisi yake kuendesha kliniki za sheria katika mikoa mbalimbali, kuandaa juzuu ya marekebisho ya sheria mbalimbali tangu mwaka 2002 na mafunzo wa mawakili wa serikali ili wawe na ubobezi katika kushughulikia mikataba mbalimbali inayoingizwa na serikali.

Akizungumzia huduma za kliniki ya sheria na mchango wake katika kutatua changamoto

za wananchi hususani wa kipato cha kawaida na cha chini katika upatikanaji wa haki, Johari anasema ofisi hiyo ilibaini kuna changamoto kubwa kwa wananchi wa kawaida hasa walioko wilayani na mikoani katika kuzifikia huduma za kisheria.

Anasema wamekuwa wakihangaika na pia gharama za kupeleka mashauri mahakamani nazo ni kubwa, hivyo wakaona umuhimu wa kuwasogelea wananchi katika mikoa na wilaya zao.

Johari anasema, “Kwa hiyo tulianzisha kamati za ushauri wa kisheria katika mikoa

na wilaya. Baada ya kuanzisha tukaziwekea utaratibu au mwongozo wa kisheria wa mwaka 2024 unaolenga kuhakikisha tunasogeza huduma za kisheria hadi ngazi za wilaya na mikoa."

Anasema moja ya nyenzo za utekelezaji wa mwongozo huo ilikuwa kuanzisha kliniki za huduma za kisheria, hasa kamati za ushauri za kisheria zinapoundwa, inaenda sambamba na wiki nzima ya utoaji wa huduma za kisheria kupitia kliniki, katika mkoa au wilaya ili kutoa huduma hizo bure.

Anasema, “Tofauti na utaratibu mwingine wowote, kliniki hizi za kisheria tunapokuwa tunatoa huduma za kisheria kwa wananchi, mwananchi yule baada ya kuwasilisha shauri lake, lalamiko lake au jambo lake lolote linalohitaji msaada wa kisheria, tukishampa ule ushauri wa kisheria hauishii pale.”

Anaongeza: “Tunaendelea naye kumfuatilia kwa sababu tunaweka rekodi kwamba shauri hili lilihusu nini, kama lilihusu ardhi basi tunaliweka katika rekodi zetu, na kutoa ushauri na pia, kuendelea kulifuatilia hata

baada ya pale mpaka likafike mwisho na suala hilo mwananchi kuwa limetatuliwa.”

Anasema kliniki hizo zinalenga kusogeza huduma za kisheria kwa wananchi katika ngazi ya mikoa na wilaya. Tayari wameifikia mikoa ya Kilimanjaro, Dodoma na Mwanza ambako wananchi wamejitokeza kwa maelfu.

“…Lengo lilikuwa kusogeza huduma karibu na wananchi tukitimiza matakwa ya Rais wetu Samia Suluhu Hassan ambaye amekuwa akisisitiza kusogeza huduma karibu na wananchi, lakini na kampeni ile

ambayo inashabihiana na hiki cha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, cha ‘Samia Legal Aid Campaign,’ lengo ni hilo la kusogeza huduma kwa wananchi,” anaeleza Johari.

Lengo la pili kwa mujibu wa Johari ni kuwapunguzia gharama wananchi.

Anasema, “Huduma hizi tunazitoa bure, kwa hiyo mwananchi anakuja anapata huduma na anaondoka”.

Anasema kuna shuhuda mmoja wa Mwanza alikuwa hajui pa kwenda na akifikiria

gharama kubwa, alipofikiwa na huduma hizi aliona kama ni nyota ya jaa.

“Kwa hiyo gharama zile tunawapunguzia kwa sababu wanakuja kupata huduma bure, na mawakili wa serikali tunawaweka pale, kwani huduma hizi zinatolewa na mawakili waandamizi wa serikali ambao ni wabobezi katika maeneo mbalimbali. Kwa hiyo wanapata huduma za kiwango cha juu bure,” anaeleza Johari.

Lengo lingine kwa mujibu wa Mwanasheria mkuu wa serikali ni kuzipunguzia mahakama

mzigo wa kesi nyingi ambazo anasema si lazima zote ziende huko.

“Inawezekana nyingine tukakaa, tukazungumza, tukawasuluhisha watu na jambo likaisha. Kwa hiyo kwa kufanya hivyo unaipunguzia mahakama mzigo mkubwa ilio nao,” anasema na kuongeza kuwa lengo lingine kuchagiza ukuaji wa shughuli za maendeleo na hivyo kuchochea ukuaji wa uchumi.

Anasema lingine ni kusawazisha uhusiano kati ya waliokuwa kwenye migogoro hiyo ya kisheria au waliokuwa wanalalamikiana, ili

wawe na amani na waishi katika amani kwa dhana ile ya haki wianishi.

Johari anasema hadi sasa utekelezaji huo wa kliniki za sheria umefikia wananchi 1,845 kwa mikoa ya Kilimanjaro, Dodoma na Mwanza.

Anazitaja kero kubwa zilizojitokeza ni ardhi ambayo imebeba malalamiko 66.

“Ardhi ni eneo ambalo kama serikali inabidi tuweze kuliangalia vizuri kwa kushauriana na wizara na wadau wengine katika masuala ya ardhi ili kuona tunapunguzaje migogoro hiyo ya ardhi,” anaeleza Johari.

Anayataja maeneo mengine kuwa ni ajira hasa katika sekta binafsi ambako waajiri wengi hawazingatia taratibu za kisheria katika masuala ya kazi na nguvu zaidi zinahitajika kupunguza kero hiyo.

Mengine yaliyolalamikiwa ni mirathi, ndoa na madai. Anasema ni jukumu la serikali kuja na mbinu za kupunguza kero hizo zikiwamo sheria na sera.

Akizungumzia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 hasa eneo la kisheria, anasema Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeshiriki kikamilifu katika utekelezaji wa maandalizi

ya dira hiyo mpya na hata ile inayomalizika mwaka huu.

Anasema, “Na pale itakapokuwa imepitishwa sasa na kuanza kutumika, basi na sisi tunaanza utekelezaji wa kuhakikisha kwamba kule tunakotaka kufika mwaka 2050, tunaweza kufika huko.”

Anaongeza: “Kwa sababu kwenye dira tunazungumza kwamba tunataka kuwa taifa ambalo litakuwa limepunguza umaskini kwa kiasi kikubwa na kuhakikisha uchumi wetu unakua na kufikia ngazi ya uchumi wa kati wa juu.”

“Sasa lengo hilo ni kubwa, lakini tunaweza tu kufanikiwa kulifikia kama tu tutahakikisha kila mdau na kila mshiriki wa maendeleo na uchumi anachukua nafasi yake stahiki na kufanya yale ambayo yanapaswa kuhakikisha sisi tunafika huko tunakotarajia kufika mwaka 2050,” anafafanua Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Anaeleza kwamba kwa kuwa dhamira ni kubwa hana wasiwasi kuwa nchi itaweza kufika huko, na hivyo ofisi yake imejipanga kuhakikisha yale yote yanayoihusu ili kufika huko 2050, wanayafanya ipasavyo.

“Baada ya kuisoma dira ile kwa kina na kuielewa jambo la kwanza ambalo Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali tutatakiwa kuhakikisha tunalitekeleza ni kuhakikisha tunaoanisha vizuri sheria tulizo nazo na kule tunakotaka kwenda,” anaeleza Johari.

Anaongeza: “Ili kufika tunakotaka kwenda, lazima kuwa na hiyo ‘legal framework’ (mpango wa kisheria) kutuwezesha kufika kule. Yaani sheria ni kama daraja la kutuvusha twende 2025 upande huu na 2050 upande ule, ni lazima tuwe na hilo daraja.”

Anasema kwa msingi huo, sheria zote lazima zioane. Anasema, “Tusipofanya hivyo, tutakuwa tunakwenda 2050, lakini sheria zinavuta nyuma.”

“Ndio maana tunafanya marekebisho ya sheria; lengo ni hilo ni ili kunyumbulika na jamii inavyokwenda, unanyumbulika na sekta za kiuchumi zinavyokwenda, unanyumbulika na changamoto mbalimbali zinavyokwenda. Kwa hiyo katika dira hii zimedadavuliwa vizuri na jinsi zitakavyokwenda ili kufika 2050,” anasema Johari.

Kuhusu kutafsiri sheria kwa Lugha ya Kiswahili, Johari anasema kazi hiyo inaendelea na kati ya Julai hadi Desemba 2024, sheria 300 zimeshatafsiriwa... Ifikapo Juni 30, 2025 tutajua zimetafsiriwa ngapi. Anasema kuanzia sasa sheria zitakuwa zinaandikwa kwa lugha zote mbili, Kiswahili na Kiingereza ili kumrahisisishia mtumiaji. Tayari ofisi yake imekamilisha urekebu wa sheria na sasa inaandaliwa juzuu ya pamoja ya kuanzia sheria zilizorekebishwa tangu mwaka 2002, ambazo sasa zitakuwa kwenye juzuu moja. Zitazinduliwa hivi karibuni.

“Rais wetu (Samia Suluhu Hassan) ametimiza jambo kubwa ambalo kwa takribani miaka 22 tulikuwa hatujafanya urekebu wa sheria. Kwa mara ya mwisho ilikuwa mwaka 2002… Safari hii tunalifanya tofauti kwa fedha zetu za ndani, huko nyuma hatukuwa na uwezo tulikuwa tunatumia fedha za wahisani,” anasema.

Anaongeza: “Tunapozungumzia urekebu wa sheria, tunazungumzia kujumuisha marekebisho mbalimbali tunayofanya kila mwaka kwenye juzuu moja ya sheria ili kumrahisishia mtumiaji wa sheria”.

*******tamati******************